**IBUA!**
#NawezaNafanyaNashinda

# KUFUNGULIA SOKO LA VIJANA: CHACHU KUU KWA MUSTAKABALI YA KIFEDHA WA TANZANIA





## HALI YA SASA

**25%** Huunda idadi ya watu wazima

**75%** Wametengwa kifedha


Vijana huchukuliwa kuwa ni soko gumu la kuhudumia kwa maana ya kutoa huduma za fedha, kwani wengi wao hawana Vitambulisho vinavyoweza kukidhi matakwa ya “Mjue Mteja Wako”, pengine hii inatokana na kiwango cha chini cha miamala inayosababishwa na viwango vyao vidogo vya ushiriki kiuchumi, hivyo kutokuwepo kwa faida zilizo dhahiri za uwekezaji kwa watoa huduma wengi.




Kwa upande mwingine, ni kundi la watu wanaokua ambao wanaweza kulelewa na kuelimishwa katika mambo ya fedha, na kulengwa kuuziwa bidhaa mseto ili kuwafanya wawe wateja wenye faida kwa kipindi chote cha maisha yao. Aidha, kama watumiaji bidhaa/ huduma wa awali kabisa, wana uwezo wa kunuifaika na fursa za teknolojia mpya.



**VIJANA** hufafanuliwa na FSDT kama watu wenye umri kati ya miaka 16 - 24 ukichukulia maanani utegemezi kiuchumi na ushiriki kikamilifu kwenye nguvu - kazi.




## Ni nani aliyetengwa?


- 79% VIJIJINI
- 76% TABAKA MBILI ZA CHINI KABISA
- 55% WANAWAKE
- 47% WAKULIMA NA WAVUVI
- 32% VIJANA (16-24)
- 24% WATAGEMEZI

## Je, wana aina yoyote ya Kitambulisho?

- Miaka 16 -24
- Miaka 25-35
- Miaka 36 na kuendelea




## Kiwango cha Upokeaji wa bidhaa za fedha




FSDT
FINANCIAL SECTOR DEEPENING TRUST

*Source: FinScope Tanzania 2017*

# MKAKATI WA VIJANA

FSDT imedhamiria kushirikiana na wadau wa umma wa huduma jumuishi za fedha kuchochea miradi matokeo, iliyo bunifu na inyoleta mabadiliko ili kukuza uwezeshaji wa vijana, kujenga uwezo na kuendeleza ujuzi.

Aidha, FSDT imeongoza miradi ya kusaidia upatikanaji wa wateja vijana ili kupata fedha na wingi wa wateja anuwai wa watoa huduma za fedha, kupunguza hatari na kuongeza ukuaji.




## Matarajio

Kuimarisha sehemu ya soko kwa ajili ya ukuaji uchumi hapo baadaye

## Dira

Vijana hunufaika kutokana na matumizi ya mara kwa mara ya huduma za fedha ambazo hutolewa kwa kuzingatia utu na haki

## Shabaha

Kupunguza pengo la upokeaji na kuongeza matumizi ya huduma za fedha na vijana ili wanufaike kutokana na huduma za fedha wanazotumia

## Dhima/ Kusudio


Sekta ya Fedha ambayo kwao wadau huelewa mahitaji na tabia za vijana na kuchukua hatua

Serikali ya Tanzania imetambua umuhimu wa vijana na kubuni Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ili kuhakikisha maslahi na mahitaji ya vijana yanaletwa mbele ili yasikike na wadau na mikakati stahiki inatolewa. Mkazo wake kwenye maendeleo ya rasilimali watu hujumuisha maendeleo ya kilimo na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na kukuza mikopo ya gharama ndogo kwa vijana, kuinua uwezo wao kwa kiwango cha juu kabisa katika shughuli za uchumi, na kuwa chachu kuu kuelekea uchumi wa viwanda na ukuaji endelevu, na kukuza masoko ya ndani na ya kimataifa kwa bidhaa zao.





Aidha, Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana iliundwa mwaka 2007 ili kuwaandaa vijana kubeba jukumu lao muhimu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Taifa kama viongozi, watoa maamuzi, wajasiriamali, wazazi na walezi.


Aidha, vijana pia wameainishwa katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano - Mpango wa II, pia katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II) kama kizazi kinachoweza kufanya vizuri. Iwapo uwezo wao hautafikiwa, hii itasababisha matokeo hasi ya uchumi wa taifa, lakini kama utaimarishwa, itakuwa chachu kuu kuelekea uchumi wa viwanda na ukuaji endelevu.



**37%** ya vijana wengi wao ni tegemezi



**57%** hutumia pesa za simu za mkononi, na vijana wanaoweka akiba, **44%** hutumia akaunti za simu za mkononi




Watoa huduma za fedha wengi huwalenga vijana kupitia akaunti zinazomilikiwa na walezi wao




**25%** wanatarajia kufukuzia taaluma amabazo zinahitaji elimu ya ngazi ya Chuo




**90%** ya vijana mijini wanamiliki simu za mkononi na **52%** wanapata intaneti



Vijana **6** kati ya **10** wanamiliki aina fulani ya kitambulisho



**54%** wanamiliki simu ya mkononi, kati ya hawa **24%** wana Simu janja



**11%** amabao wanadai kumiliki ardhi binafsi, ni **2** kati ya **10** wenye ushahida halisi wa umiliki

IBUA! #NawezaNafanyaNashinda

FSDT FINANCIAL SECTOR DEEPENING TRUST

*Source: FinScope Tanzania 2017*